

LBE 2009 – Migration

Episode 10: A German in Uganda

Author : Adrien Demun

Editor : Thomas Mösch

Translator :

1 Narrator

3 Voice-overs: - Roberta Wagner, female, 31 yrs

- Sarah Nagire, female

- Peter Mubanda, male

Intro

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga maisha Yako kuhusu uhamiaji kati ya Afrika na Ulaya. Leo hii tunakujulisha kwa mtu ambaye amehamia kinyume na tulivyozoea kila siku. Yaani kutoka Ulaya kwenda Afrika.

1. Narrator:

Watu wanaohamia kutoka nchi za nje kwenda Afrika hawaitwi wahamiaji bali wao huitwa wataalamu. Wengi wao huenda huko kwa ajili ya kazi maalum na baada ya hapo huondoka. Lakini wengine wao huamua kubaki, kama Roberta Wagner. Aliondoka Ujerumani miaka tisa iliyopita, kuishi nchini Uganda, nchi isiyo na bahari huko Afrika Mashariki. Wala hana mpango, kwa sasa wa kurudi kuishi Ujerumani. Roberta ana kazi nzuri, yeye ni mkurugenzi wa chama cha ushirikiano wa kitamaduni baina ya Ujerumani na Uganda. Leo anatayarisha tamasha la muziki pamoja na bendi ya muziki ya nyumbani. Lakini, kama ilivyo kawaida katika mji wa Kampala, umeme ulikatika punde tu kabla ya tamasha hilo kuanza.

2. SFX Sound of generator

3. Roberta Wagner

Nisemeje! Umeme umekatika! Kwa kawaida hilo huwa halitokei hapa Nakasero, lakini ni jambo la kawaida nchini Uganda. Sasa tuombe tu umeme urudi, vinginevyo tutaendelea hivyo hivyo bila umeme, Kwa sababu jenereta yetu si kubwa kiasi cha kumudu mfumo wa vipaza sauti.

4. SFX Steps

5. Narrator:

Roberta Wagner anaelekea kwenye chumba chenye giza waliko wanamuziki ambao wanasubiri.

Dialogue Roberta and Sarah Nagire

6. Roberta:

“Nauliza tunaweza...kama tukiweka taa za mafuta kwenye mitungi mbele ya jukwaa, je. Tunaweza kuendelea kucheza muziki bila umeme?”

7. Sarah Nagire:

“La, haiwezekani kwa sababu hatukupanga. Hatuwezi. Pia hatuna jenereta. Hatuwezi kufanya lolote. Sina fedha za kukodisha jenereta. Sina kabisa”.

8. Roberta:

“Hapana, hapana... nina maana, tuchezeshe vyombo bila umeme?”

9. Sarah: “uh uh”

10. Roberta:

“Sijui la kufanya...Tuombe. Unaweza kuomba?”

11. Sarah:

“Niliomba na mvua ikapotea. Na sasa bado nazidi kuomba ili umeme urudi...shida gani hii!”

12. Narrator:

Baada ya robo saa, umeme unarudi, na wanamuziki wanapanda jukwaani. Roberta Wagner, anapata utulivu, na hapo anatoa hotuba ya makaribisho.

13. Roberta Wagner

Tumemkaribisha Sarah Nagire jioni ya leo kwa sababu yeye ni mwanamke mkakamavu. Anaimba kuhusu amani, uhuru na haki za binadamu. Nina hakika tutakuwa na jioni njema yenye furaha. Ninatumai kuwa mtaupenda muziki wake. Pia nina matumaini kwamba mtafurahia mchanganyiko wa muziki wa kienyeji na muziki wa kisasa. Ninafuraha kwamba sasa tunaweza kuanza, na ninafuraha kuwa umeme umerudi, lakini natumai utaendelea kuwepo bila kukatika tena. Tafadhalini sana, iwapo umeme utakatika, msiwalaumu Wajerumani. Ninawatakia furaha, tafadhali mpigieni makofi Sarah Nagire na bendi yake.

14. SFX Applause (from archive)**15. Sarah Nagire**

Kifuatacho, mabibi na mabwana, ni wimbo mzuri, wimbo mfupi ambao unatoka kwenye alamu yangu ya pili. Na wimbo huu unaelezea, hususan kwa nini ninaimba, na kwa nini wengi wetu tulio hapa jioni ya leo huwa tunaimba. Natumai mtaburudika.

16. MUSIC

17. Narrator:

Asubuhi iliyofuata, Roberta Wagner, akiwa bado ana machofu, amerudi ofisini mwake, katikati ya jiji la Kampala. Anatumia ofisi hiyo pamoja na kituo cha utamaduni cha Ufaransa.

18. SFX Roberta walking. She opens her door.

19. Roberta Wagner

Hii ni ofisi yangu, ambako ninafanyia shughuli zangu za kila siku, mahala ambapo ninaweza kubuni mawazo yangu yote kwa utulivu. Ya...Na pia nina bango lenye picha ya Barack Obama ambayo inanikumbusha – kila siku, nikija ofisini naiangalia, Inanikumbusha jinsi dunia inavyobadilika hivi sasa - .

20. Narrator:

Roberta Wagner anauona ushindi wa Barack Obama kama ni ushindi wake binafsi pia.

21. Roberta Wagner

Nimekulia kwenye familia ambayo ina mchanganyiko wa tamaduni, baba yangu wa kambo ni Mmarekani mweusi, kwa hivyo nafikiri kwa Mmarekani mweusi kuingia ikulu hayo ni mafanikio makubwa, nafikiria ... baba yangu alinipigia simu siku ile Obama alipochaguliwa, alikuwa analia. Na alisema, “Sikudhania kama mwafrika mweusi ataingia ikulu”. Kwa sababu...nina maanisha jinsi alivyolelewa, hilo lilikuwa ni jambo ambalo haliwezekani. Na kwa watu ambao wamefikwa na vitendo vya ubaguzi, hayo ni mabadiliko. Tena mabadiliko makubwa. Ni wazi kwamba Obama anakabiliwa na changamoto nyingi kwa sasa kwa sababu anatarajiwa kuubadili ulimwengu, na huo ni mzigo mzito,

nafikiri. Kwa hiyo watu watawunjika moyo kwa sababu hataweza kutimiza kila kitu kile ambacho watu wanamtegemea kukitimiza. Lakini, angalau, kwa mtu mweusi kuwa rais wa Marekani...nafikiri rais atakayefuata atakuwa ni mwanamke. Kweli, dunia inabadilika.

22. Narrator:

Wakati Roberta Wagner alipofika Uganda ilikuwa ni mara yake ya kwanza kufika Afrika na anakumbuka vyema mawazo yake ya kwanza.

23. Roberta Wagner

Tulifika usiku, na tuliendesha kutoka Entebbe, kutoka uwanja wa ndege mpaka Kampala, ni kama muda wa dakika 40 hivi kwa gari. Na wakati huo, tuliambiwa kuwa barabara hiyo ilikuwa hatari. Tuliambiwa kuwa kuna wezi wanaoteka magari na watu wanaotaka...kwa sababu wanajua kuwa mnatoka uwanja wa ndege. Kwa hiyo mna fedha nyingi na vitu vya thamani...kwa hiyo...kwa vyovyote vile, watu walikuwa wananiambia juu ya hofu waliyonayo walipoendesha katika barabara hii. Lakini kwangu mimi, nilipoingia kwenye taxi, hata sikuvingiwa na uoga huo. Niliwaona watu barabarani. Maisha ya kawaida, rangi. Pia kulikuwa na giza, lakini uliweza kuona ile tofauti, ukitokea Ujerumani. Ujerumani ambako...nina maana...ikifika saa nne usiku, huwezi kuona mtu barabarani. Lakini nilipofika Kampala, unajua, maisha yako usiku tena barabarani. Na hilo lilinipa mtazamo wa ndani sana.

24. Narrator:

Ni mapenzi, ndio yaliyompeleka Roberta Wagner Afrika.

25. Roberta Wagner

Nilipokuja Uganda nilikuwa mdogo sana. Ni miaka 10 au 9 iliyopita, nilikuwa nina miaka 21 na nilikuwa bado nasoma huko Ujerumani.

Nilikutana na mwanamume huko huko Ujerumani. Na yeye alikuwa mwanafunzi pia, tulikuwa tunasoma pamoja katika chuo kikuu, alipata kazi Uganda. Na alinitaka nijiunge naye.

26. Narrator:

Huko Uganda Roberta alifunga ndoa na mpenzi wake huyo Mjerumani mwenzie, baada ya hapo alipata mtoto wa kiume.

27. SFX a spoon in a cup of coffee

28. Roberta Wagner

“Hi hi, Kahawa”

29. Roberta Wagner

Tulipokuja Uganda mara ya kwanza, tulikwenda Fort Portal. Huko ni mpakani mwa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, tulikaa huko kwa miaka miwili, halafu tukahamia Kampala na Kampala kukawa ni mahala paliponifurahisha sana na ndipo nikawa mwanachama wa chama cha ushirikiano wa kitamaduni baina ya Uganda na Ujerumani. Nilisomea usanii katika chuo kikuu cha Makerere. Nilijihusisha sana na shughuli za utamaduni. Na hapo niligundua kuwa hilo hasa ndilo nililotaka kulifanya. Nilihisi kuwa ninaweza kuleta mabadiliko au ninaweza kusaidia kuleta mabadiliko hayo. Ninaweza kuunga mkono shughuli za usanii. Nilipoanza kufanya kazi katika kituo cha utamaduni cha Ujerumani hapa mjini Kampala, nilijua haitakuwa rahisi kwangu kwenda mahala pengine. Nina shughuli nyingi Uganda. Nina mpenzi, nina mtoto, nina familia na nina kazi. Hakuna sababu ya kunifanya niende kwingine.

30. Narrator:

Maisha ya Roberta Wagner nchini Uganda hayakuwa mazuri wakati wote. Fort Portal ilikuwa mwanzo wa maisha yake. Halafu akaachana na mumewe Mjerumani. Sasa anaishi na mpenzi wake Mganda, lakini Mganda huyo sio wa kawaida. Mpenzi wake huyo, Peter Mubanda, alizaliwa na kukulia New York, na baadaye akaamua kurejea nchi alikotokea.

31. Peter Mubanda

(transcription not literal but trying to bring out the meaning of what he says)

Roberta si Mjerumani wa kwanza kufanya naye urafiki, kw ahiyo nawafahamu vyema Wajerumani. Maswala ya tabia ..tamaduni...yote haya...huenda yakawa ni maswala magumu hapa Afrika...Labda kwa sababu ya... mazingira ya kijamii na kiuchumi, na mtazamo wa Waganda asilia na kama ujuavyo, swala la watu weusi na weupe. Mambo kama hayo...lakini jambo la kufurahisha ni kwamba, yeye huenda amekaa muda mwingi katika nchi yangu kuliko mimi...Kwa hiyo, bila shaka ameona mengi kwenye nchi yangu kuliko mimi...na kwa sababu hiyo, yeye ni Mganda zaidi kuliko mimi... *(stuttering)*

32. Narrator:

Roberta Wagner anaonekana kuwa anayafurahia maisha yake mapya ya Afrika pamoja na mpenzi mpya aliyempata. Mara moja moja anakumbuka maisha yake ya Ujerumani na hapo hushikwa na majonzi.

33. Roberta Wagner

Ninaikumbuka familia yangu na chakula. Hivyo ndivyo vitu viwili ninavyovikumbuka sana. Hasa mikate, na Soseji. Ninakumbuka pia utamaduni wangu. Ninakumbuka wakati wa kwenda kwenye tamasha

zuri, ...na rafiki zangu. Kuna mambo mengi ninayoyakumbuka, hiyo ni hakika. Ujerumani ni nyumbani, ni nchi yangu ya utambulisho, mimi ni Mjerumani hata nikijibadili vipi. Mizizi yangu ni hiyo na mtu hawezi kusahau mizizi yake ilikotoka. Hivyo ndivyo nilivyo.

34. Narrator:

Licha ya yote hayo ambayo Roberta Wagner anayakumbuka kuhusu nchi yake Ujerumani, anapata shida kukubaliana na hali ya uraia wake.

35. Roberta Wagner

Mara nyingine, hugundua kuwa mimi tayari ni Mganda zaidi kuliko Mjerumani, kwa sababu nikipata wageni kutoka Ujerumani, wananiuliza maswali mengi. Kwa nini iwe hivi hapa Uganda? Hapo hufahamu kwamba kwangu mimi hilo si jambo geni. Linakuwa ni jambo geni kwangu, wakati ninapokuwa Ujerumani kwa sababu lazima nipange miadi ninapotaka kukutana na watu. Ujerumani mambo mengi ni tofauti kabisa. ninajihisi mimi ni sehemu ya jamii hapa.

Outro:

Na mpaka hapo ndio tumekamilisha makala ya leo katika Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu uhamiaji. Makala ya leo imeandikwa na Adrien Demun. Iwapo ungetaka kujifahamisha zaidi kuhusu kipindi hiki au kuhusu kipindi kingine chochote katika makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako, ama kama unataka kukisikiliza tena kipindi cha leo, tafadhali tembelea tovuti yetu. Anuani yetu ni: www.dw-world.de/lbe Asante kwa kuwa nasi. Hadi wakati mwingine. Kwaheri.